

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA MWANZA:
Anuani ya Simu: "ADMIN"
Simu Nambari: 028-2515056
Tovuti: www.mwanza.go.tz
Barua Pepe: das.ukerewe@mwanza.go.tz



OFISI YA MKUU WA WILAYA,
S.L.P.02,
NANSIO/UKEREWE.

Unapojibu Tafadhali Taja:

Kumb. Na. AB. 46/367/01/14

19/07/2022

**TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI WA MAKARANI WA SENSA,
WASIMAMIZI WA MAUDHUI NA WASIMAMIZI WA TEHAMA.**

1. Mwenyekiti wa Kamati ya Sensa Wilaya ya Ukerewe anawataarifu wananchi wote walioomba ajira za muda za kazi ya sensa ya watu na makazi itakayofanyika tarehe 23 Agosti, 2022 kuhudhuria kwenye usaili utakaofanyika katika maeneo yao waliyoombea.
2. Usaili utafanyika tarehe 22/07/2022 kuanzia saa 2:00 asubuhi katika maeneo ya shule za Sekondari za Kata kwa nafasi ya Karani wa Sensa na Msimamizi wa maudhui. Kwa nafasi ya Msimamizi wa TEHAMA usaili utafanyika katika Ukumbi wa Halmashauri kwa tarehe tajwa hapo juu.
3. Waombaji wote mnajulishwa kufika na nyaraka halisi zilizotumika kuomba nafasi ya kazi siku ya usaili.
4. **Orodha ya Majina ya wanaoitwa kwenye usaili yameambatishwa na barua hii.**

Col. Denis F. Mwila
MWENYEKITI WA KAMATI YA SENSA (W)
UKEREWE.

